

MBAO ZA MATANGAZO NA TOVUTI YA HALMASHAURI

(TAREHE 27.06.19)

YAH: UJAZAJI WA OPRAS KWA WATUMISHI MWAKA 2018/2019

Husika na mada tajwa hapo juu.

OPRAS ni fomu ya wazi ya tathmin na upimaji utendaji wa kazi kwa wafanyakazi, ambayo inakusudiwa kukidhi mahitaji ya mfumo wa upimaji wa utendaji kazi ambayo ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria No. 8/2002, hivyo kujaza **OPRAS** siyo hiyari ya Mtumishi.

Ni kwa misingi hiyo Watumishi wote wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi mnaelekezwa yafuatayo:-

- i. Kwa Watumishi wasio Walimu darasani wakamilishe tathmini ya **OPRAS** ya mwaka 2018/2019 ifikapo tarehe 30/06/2019.
- ii. Kwa Watumishi wasio Walimu wa darasani wajaze **OPRAS** (Malengo) na kukubaliana na wasimamizi wao.
- iii. Watumishi Walimu wa darasani wafanye mapitio ya nusu mwaka ifikapo tarehe 30 Juni, 2019.

NB:

Ukaguzi wa ujazaji wa **OPRAS** utafanyika kuanzia tarehe 01/07/2019 na baada ya hapo orodha ya Watumishi ambao hawatakuwa wametimiza takwa hili la Kisheria itawekwa katika tovuti na hatua za nidhamu zitafuata kwa mujibu wa Sheria.



Mwangalika, F.J
Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala
MASASI